BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

Simu ya Upepo: Baraza
Nambari ya Simu:2230234/5
Tele Fax. Nam. (024)2230215

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA (P.A.C) YA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR, 2011.

SEHEMU YA KWANZA:

1.0 UTANGULIZI:

Kwa mnasaba na Mabadiliko ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2011, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika imeundwa na kupangiwa majukumu yake chini ya Kifungu cha 115. Majukumu hayo ni haya yafuatayo:

- Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- Kuchambua na kutafakari ripoti yeyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.
- Kuchunguza kwa njia yeyote inayoona mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na asasi zake.
- Kutoa Ripoti yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.
- Katika kufanya kazi zake Kamati ya PAC itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama:
  Fedha zilizooneshwa katika makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama iliyvo kubaliwa na matumizi yalikuwa chini ya mamlaka iliyohusika na Matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

1.1 UPEO WA KAZI:

Kutokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya mwaka 2008/2009 kuwasilishwa katika kikao hiki cha March 2011, Kamati ya P.A.C kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 115

(2) (c) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2011, imeamua kufuatilia maagizo yaliyotolewa na Kamati za miaka ya nyuma, kuanzia mwaka 2006/2007; 2007/2008; 2008/2009 na 2009/2010. Aidha, kazi hii imefanywa kwa Wizara 8 zifuatazo:

- Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
- Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.
- Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
- Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
- Wizara ya Afya.
- Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Ifahamike kwamba, kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Kamati imezifanyia kazi Taasisi zinazohusika na Utalii pekee.

1.2 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UFUATILIAJI WA MAAGIZO YA KAMATI:

Baada ya kufuatilia maagizo hayo, mambo yafuatayo yamebainika:

Serikali kutofuatilia Ripoti za Kamati:

Bado tatizo la Serikali kuzifuatilia na kuzifanyia kazi Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza baada ya kuwasilishwa Barazani linaonekana kuendelea. Katika kazi za Kamati, Taasisi nyingi hazikuwa na hata Ripoti za Kamati na matokeo yake watendaji wake wanaohusika na fedha, wamelazimika kutafuta angalau kopi zinazohusu maagizo ya Taasisi zao kupitia Makatibu wa Kamati. Kwa upande mwengine, maamuzi ya Kamati kufuatilia maagizo iliyoyatoa katika ripoti zilizopita, kumewafanya watendaji wa Serikali angalau kuamka na kuona umuhimu wa kuwa na Ripoti za Kamati na kuzifanyia kazi.

Kukamilika kwa Mfumo mmoja wa kuhifadhia kumbu kumbu za Mali za Serikali (Assets Registrer):

Kwa miaka mingi sasa Kamati imekuwa ikiitaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kukamilisha mfumo mmoja wa kuhidadhia mali za Serikali (Assets Registrer). Tatizo liliopo kwa muda mrefu ni kwamba, Taasisi za Serikali hazina kumbu kumbu ya mali wanazozimiliki na kila Kamati ilipofuatilia suala hili, ilipewa majibu ya kusubiri muongozo mmoja kutoka Wizara husika. Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, imeifahamisha Kamati kwamba tatizo hili sasa limeshaondoka na kwa msisitizo, Kamati ilifanya kikao cha

Majumuisho ya kazi na Taasisi zote zilizohusika kwa lengo la kupeana habari na kuwataka warekebisehe kasoro zilizokuwepo kabla.

Kukosekana kwa Hati Miliki za Ardhi za Serikali:
Bado tatizo la kukosekana kwa hati miliki kwa mali za Serikali linaendelea. Kinachoishangaza Kamati ni kwamba, maombi ya kupatiwa hati hizo kwa Taasisi za Serikali yanachelewa wakati Taasisi za watu binafsi zinapata wepesi wa kumiliki hati hizo. Kwa hili bila shaka matatizo yako ya pande mbili, moja ni Taasisi zenyewe haziombi hati miliki wala hazifuatilii kabisa na tatizo la pili ni Wizara inayohusika na Ardhi, huwa na urasimu mkubwa wa kutoa hati hizo. Kwa mfano, Shirika la Bandari, Wizara ya Kilimo na Taasisi nyengine kama zilivyoripotiwa katika ripoti hii, zinaieleza Kamati kwamba wameshapeleka maombi na kukamilisha taratibu za kuomba hati hizo ila bado hawajapatiwa. Kamati inaitaka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilishughulikie tatizo hili.

Uwezo wa Mashirika kujiendesha kwa Faida:
Kuna matatizo makubwa kwa Mashirika mengi ya Serikali, Kamati inaona bado Serikali haijamaliza kazi ya kuyaimarisha Mashirika yake. Mifano inaonekana kwa Mashirika kadhaa yakiwemo Shirika la Utalii, Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na Mashirika mengine. Kinachoipa matumaini Kamati ni kuahidiwa kuwepo Mabadiliko ya Mfumo wa Mashirika “Reform” kwa lengo la kuyawezesha kujiendesha kwa faida. Kamati inasubiri kukamilika kwa “Reform” hiyo na kufanyiwa kazi.

Ukaguzi wa Vielelelezo vinavyotolewa maagizo na Kamati:
Katika utekelezaji wa kazi hizi, Kamati imebaini kwamba kuna Taasisi nyingi huionesha Kamati vielelezo vilivyokosekana wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu. Baada ya kuonekana mbele ya Kamati, mara nyingi Kamati huwaagiza wawasiliane na Afisi ya Mdhibiti ili avikague na hatimae waijuilishe Kamati. Tatizo liliopo ni kwamba, Taasisi nyingi hudharau kutekeleza maagizo haya na mara nyengine hutekeleza nusu ya agizo, yaani huwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu bila ya kuijuilisha Kamati hatua iliyofikiwa. Kamati inaziagiza Taasisi za Serikali kurekebisha Kasoro hii.

1.3 WAJUMBE WA KAMATI:

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika kwa mwaka 2011, inundwa na Wajumbe 8 na Makatibu 2. Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Omar Ali Shehe	Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Mjumbe
4. Mhe. Farida Amour Mohammed	Mjumbe
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman	Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Mjumbe
9. Ndg. Abdalla Ali Shauri	Katibu
10. Ndg. Othman Ali Haji	Katibu

1.4 UHUSIANO ULIOPO BAINA YA KAMATI YA PAC NA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR.

Kuna mahusino makubwa na ya karibu baina ya Kamati na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar. Jukumu kubwa la Kamati ni kuchunguza na kutoa taarifa baada ya kufuatilia hoja zilizohojiwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu juu ya mapato, matumizi na ufanisi wa shughuli za kifedha serikalini.

kwa vile kamati hutegemea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu katika kutekeleza majukumu yake, kunahitajika maelekezo na uchanganuzi yakinifu wa ripoti hizo ili upatikane ufanisi wa kazi hiyo njia mbali mbali za kuijengea uwezo Kamati na Afisi ya Mdhibiti inahitajika kutumia mbinu mbali mbali za kuijengea uwezo utakaosaidia kuwapatia taaluma wajumbe wa Kamati juu ya tafsiri, dhana, taratibu na sheria za kifedha hali ambayo husaidia uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuifahamisha jamii jinsi gani Afisi ya Mdhibiti inadhibiti na kuzikagua hesabu za Serikali. Aidha, Kamati kupitia ripoti na kazi zake huainisha na kutoa changamoto mbali mbali kwa Afisi hii ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

Miongoni mwa changamoto zinazoikabili Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ni kuwepo maslahi madogo ya watendaji wake. Inasikitisha sana unapoikuta Afisi hii ina kazi ngumu ya kuzichunguza, namna gani fedha za umma zimetumika, uhalali wa

matumizi yake kama zilivyoidhinishwa na kwa kuzingatia thamani halisi ya matumizi ya fedha hizo katika ujenzi wa Taifa, wakati huo huo maslahi ya watendaji wa kazi hizi za uchunguzi na udhibiti wa fedha za umma ni madogo mno ukilinganisha na baadhi ya taasisi wanazozikagua.

Hali ya udogo wa maslahi katika Afisi hii inaweza kupelekea kuondoa motisha kwa watendaji, jambo ambalo linaweza likaashiria vishawishi na tamaa mbali mbali na kupunguza ufanisi na uwajibikaji wa Afisi. Pamoja na hali hiyo bado watendaji wa Afisi hii wanaonesha uzalendo na wanafuata vyema maadili ya kazi zao.

Tunaipongeza Serikali kwa kufahamu umuhimu wa kuimarisha maslahi ya watendaji wa Taasisi nyengine za Serikali zinazohusika na ukusanyaji wa fedha za umma. Kwa mfano, watendaji wa Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) wanajisikia kutekeleza majukumu yao ipasavyo, kwa sababu Serikali imeimarisha maslahi ya watendaji hawa. Hata hivyo, Kamati yetu inasikitishwa na hali ndogo ya kimaslahi iliyopo kwa watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ambao wanafanya kazi ngumu zaidi ya kuzisimamia na kuzidhibiti fedha za umma .

Changamoto nyengine inayoikabili Afisi hii ni kuwepo mapungufu mengi ya kiutendaji katika sheria yake namba 11 ya 2003 ya Uanzishwaji Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Ambapo kuna baadhi ya vifungu vya sheria hiyo vinapingana na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 112, sheria za kimataifa za ukaguzi na sheria ya fedha namba 8 ya mwaka 2005.

Kwa kuzingatia maelezo haya, Kamati inaiomba serikali iangalie kwa kina Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na iwezeshwe kwa kuiongezea bajeti yake ya kazi za kawaida, kuwapa fursa zaidi za masomo na kuinua maslahi ya wafanyakazi wa Afisi hiyo, ili Afisi iweze kutimiza malengo yake iliyojipangia ikiwemo ukaguzi wa ufanisi (VFM), Ukaguzi wa Mazingira, Ukaguzi wa Kompyuta n.k kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla. Hili sio tu kama litaisaidia Serikali peke yake, lakini pia litaifanya Kamati kupata faida nyingi sana ikiwa ni pamoja na Afisi kuweza kufanya ukaguzi yakinifu (value for money) wa matumizi mbali mbali ya Serikali kwa muda muafaka na hivyo, uwajibikaji wa Serikali utaweza kuonekana kwa wananchi kupitia ripoti mbali

mbali za kila mwaka na ripoti nyengine zitakazofanywa inapotokea haja ya ukaguzi maalum.

SEHEMU YA PILI:

2.0 UFAFANUZI WA MAAGIZO YALIYOFUATILIWA NA KAMATI KWA WIZARA NA MASHIRIKA YA SERIKALI:

2.1 WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Agizo Nam. 1:

Kamati iliishauri Wizara kuzifuatilia nyumba za Shirika la Utalii zilizoko Chwaka,

Jambiani na Makunduchi zilizopewa taasisi nyengine, zirejeshwe ili Shirika liweze

kuzitumia. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-323).

MAPITIO YA KAMATI

Kamati iliarifiwa kwamba kuhusu nyumba za Chwaka, Mhe. Rais wa wakati huo aliagiza nyumba hizo zikabidhiwe Serikali ya Mkoa wa Kusini kwa kuzikarabati na kuzizungushia uzio “Fance”, kama Kamati ilivyopatiwa ushahidi wa agizo hili kupitia barua ya Katibu wa Zamu, Ndg. Saleh Sadiq Osman, ya tarehe 16 April, 1997 yenye kumbu kumbu namba WAU/Z.10/5. Hata hivyo, Serikali ya Mkoa huo ilizikabidhi kwa uongozi wa Chuo Cha Fedha, ambapo nyumba moja tu ndiyo iliyofanyiwa ukarabati na kutumiwa na Chuo na nyengine iko katika hali mbaya mpaka leo.

Aidha, kwa upande wa nyumba za kusini (Makunduchi na Jambiani), baadhi ya nyumba hizo, ziko mikononi mwa Shirika na nyengine haziko katika hali nzuri kwa kukosa kushughulikiwa.

Kamati imearifiwa kwamba Serikali inataka kuwapa vikosi vya serikali.

MAONI YA KAMATI

Kuhusu Nyumba za Chwaka, Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kukusu umiliki na mtumiaji halali wa nyumba hizo. Ili kujiridhisha, kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha, 2005, Kamati inatarajia kukutana tena na Uongozi wa Shirika la Utalii, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Idara ya Uhakiki mali na Mitaji ya Umma, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini na Uongozi wa Chuo cha Chwaka, ili kufahamu khatma ya nyumba hizo.

Kwa kuwa kamati iliarifiwa kwamba shirika linataka kuzitumia nyumba hizi hususan nyumba za kusini ambazo kwa sasa hivi hazitumiki ipasavyo,Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuzirejesha nyumba kwa Shirika ili Shirika liweze kuzitumia, hali hii italisaidi kulijengea Shirika uwezo zaidi wa kujiendesha.

Agizo Nam. 2

Kamati iliagiza Wizara kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifanye ukaguzi kuhusu hati za malipo ya shughuli mbali mbali zilizokosekana zenye thamani ya Tsh 440,000/= (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-324).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati iliarifiwa kwamba baada ya kasoro hizo Wizara iliwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na hatimae hoja hiyo ikafutwa.

MAONI YA KAMATI:

Baada ya kupata vielelezo na kujiridhisha kutoka Wizarani pamoja na Afisa Mkaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti, kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha, 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Agizo Nam. 3

Kamati iliagiza Wizara iwasiliane na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani (store ledger) wakati wa ukaguzi na hatimae Kamati ijuilishwe. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/10, uk-89).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati iliarifiwa kwamba Wizara imefanya utaratibu wa kusajili mali lakini bado hawajakamilisha huku wakisubiri mwongozo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

MAONI YA KAMATI:

Kamati inapongeza kwa hatua zilizochukuliwa kwa hatua iliyofikiwa na inaagiza zoezi likamilike kwa sababu tayari Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeshatoa mwongozo huo na hivyo, Wizara haina sababu ya kujitetea juu ya hilo.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Kamati imehoji kuhusu ununuzi wa gari ya Afisa Mdhamini, ambapo Wizara imekiri kununua gari hiyo kwa Tsh.22,000,000/- na iko katika utaratibu wa kusafirishwa kupelekwa pemba na hatimae kutumiwa na Afisa Mdhamini, ambae kwa sasa hana gari. Hata hivyo, Kamati inahitaji kupata ufafanuzi wa kina kuhusu taratibu za ununuzi wa gari hiyo. Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za mwaka, 2005, Kamati inahitaji kulifanyia kazi zaidi suala hili. Hivyo, Kamati inaiagiza Wizara kutayarisha "Documents' zote zinazohusika na ununuzi wa gari hiyo ili ziweze kupatikana wakati wa kazi hii. Kwa vile kuna tetesi zinazoeleza kwamba gari hiyo ilikuwa ya Serikali baadae akauziwa mtu binafsi na baadae tena kununuliwa na Serikali.

2.2 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC):

Agizo Nam. 1.

Kamati ililiagiza Shirika kufanya marekebisho ya mfumo wa utawala ili liweze kujiendesha kwa faida. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-107).

MAPITIO YA KAMATI

Kamati imearifiwa hatua mbali mbali ambazo Shirikia inazichukuwa katika kufikia azma ya kujiendesha wenyewe, miongoni mwa hizo ni pamaoja na kupunguza wafanyakazi kutoka 279 hadi 260, Shirika limeanza kupunguza kujiendesha kwa utegemezi wa mkopo kutoka Benki ambao unaathiri sana Shirika kutokana na riba ya mkopo huo, Shirika pia limepanga kupunguguza idadi ya magari Unguja na Pemba, aidha Serikali kupitia Wizara inatayarisha mageuzi (reform) ili kuliwezesha Shirika lijiendeshe vizuri.

MAONI YA KAMATI

Pamoja na jitihada hizo zinazochukuliwa kuliimarisha Shirika kiutendaji, Kamati bado haijaridhika na mwenendo wa Shirika, hivyo inaiomba Serikali kupitia mageuzi (reform)hayo yanayoandaliwa, ichukuwe dhima ya kuhakikisha inaliweka Shirika katika kiwango kizuri cha ufanisi ikiwa ni pamoja na kuliwezesha kujiendesha wenyewe.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Kamati imehoji deni la Shirika la Tsh. Bilioni 4.8 ambalo Shirika ilikuwa inalidai Serikali na kufahamishwa kwamba wamelipwa Tsh. Bilion 1.5 tu na deni lilosalia limesamehewa. Kamati ilitaka ufafanuzi zaidi kuhusu suala hili na kuwaita Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Fedha na uchumi, Meneja Mkuu wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na watendaji wake, ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusu suala hili. Aidha, Kamati imefahamishwa kwamba deni hilo ni la muda mrefu lililosababishwa na Serikali kujiendesha zaidi kwa kutegemea mapato ya Karafuu yaliyokusanywa na Shirika. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 80, Serikali ilianza Kujivua moja kwa moja na utegemezi huu na hakukuwa na uwezo wa moja kwa moja kwa Serikali kulilipa lote wakati mmoja, na hivyo kwa kufuata taratibu

na kuomba idhini Serikalini, ikaamuliwa kulipa Bilioni 1.5 kwa wakati mmoja ili Shirika liweze kujiendesha na deni lilobakia ni kusamehewa.

Kwa kuwa hakukuwa na njia nyengine zaidi ya hii, na kama Kamati itailazimisha Serikali iwalipe Shirika huku Serikali nayo ikatilia maanani kulipwa kodi zote za uendeshaji wa Shirika, bila ya shaka hakutakuwa na msaada kwa Shirika, na hivyo, Kamati imeupokea uamuzi huo. Hata hivyo, inasisitiza kwa Serikali kuyaangalia na kuyaimarisha Mashirika yake.

Kamati ilipata taarifa kwamba Wizara imenunua gari lenye thamani ya Tsh 23,500,000/- kwa ajili ya kazi za ukaguzi. Kwa kutaka kujuwa uhalali wa manaunizi hayo Kamati iliagiza Wizara kuwapatia vielelezo vyenye kuonesha utaratibu mzima wa manunuzi hayo.Kamti imepatiwa baadhi ya vielelzo hivyo ikiwemo invoice pamoja na barua ya maombi ya ununuzi wa gari hilo ambayo Afisa Biashara na Masoko wa Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko Ng. Sabri M. Muumini alimuandikia Katibu Mkuuwa wa Wizara hiyo kuomba ruhusa ya ununuzi wa gari hilo. Hata hivyo Kamati haijaridhika na vielelezo hivyo kwani kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma thamani ya pesa ambayo imenunuliwa gari hilo inalazimisha kufuatwa kwa taratibu za 'Tender' kwajili ya manunuzi hayo, ufafabuzi ambao Kamati haikuweza kupatiwa. Aidha Kamati iliarifiwa kwamba gari hilo limekusudiwa kwaajili ya matumizi ya Afisa Mdhamini Pemba wakati Barua iliyowasilishwa kwenye Kamat inaonesha kwamba gari hilo lilikusudiwa kutumiwa na Idara kwa ajili ya kazi za Ukaguzi. Hivyo Kamati inamashaka na utaratibu mzima wa ununuzi wa gari hilo na kwa maelezo haya Kamati inaitaka Wizara kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu suala hili.

Kamati imefahamishwa kwamba, Serikali iko katika hatua ya kuliimarisha Shirika kupitia "Reform" itakayoliwezesha Shirika kujiendesha kwa faida na kujitegemea. Kamati imelipokea hili na kuitaka Serikali iharakishe kumalizika kwa Reform hiyo.

3.0 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

3.1 HOTELI YA BWAWANI:

Agizo Nam. 1:

Uongozi wa Hoteli utafute Mkaguzi wake wa ndani na kukamilisha kasoro zilizojitokeza katika hoja nam. 39.1 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-90).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imearifiwa kwamba tayari hoteli imemuajiri mkaguzi wa ndani.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imeridhika na hatua ya Hoteli kumuajiri Mkaguzi wa ndani ili kuondosha kasoro zilizojitokeza. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na hali kijumla ya uendeshwaji wa Hoteli hiyo ambapo Hoteli inazidi kushuka hadhi yake kutokana na uendeshaji mbovu.

Agizo Na. 2

Kamati iliagiza kufuatiliwa kwa madeni yenye thamani ya Tsh 21,779,600/= yanayodaiwa taasisi mbalimbali. (Agizo hili linatokana Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-90).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imearifiwa kwamba bado madeni hayo hayajalipwa ingawa Taasisi zinazodaiwa zimeahidi kulipa madeni hayo.

MAONI YA KAMATI:

Kamati haikuridhika na hali hii hususan ukizingatia kwamba Taasisi hizo zinaendelea kupata huduma Hotelini hapo, hivyo imeutaka Uongozi wa Hoteli kuyafuatilia madeni hayo.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Hoteli ya Bwawani haiko katika hali nzuri ya kiuendeshaji, kwa muda mrefu imekuwa ikizidai taasisi nyingi za Serikali ambazo hupata huduma hapo na bado fedha hizo hazijalipwa. Kinachoonekana ni kwamba, Hoteli imekuwa kama ni chaka la baadhi ya watu hususan viongozi na Taasisi za Serikali kuitumia kwa maslahi yao binafsi na kuamini kwamba wana haki ya kuitumia bila hata ya kulipa gharama zozote.

Ili kuondosha kasoro zilizopo, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuifanya Hoteli ya Bwawani kuwa Shirika linalojitegemea na kuliwezesha kujiendesha kama yalivyo Mashirika mengine ya Serikali.

Miongoni mwa mambo yaliyofahamika ni kuwepo kwa utata katika ukodishaji wa kumbi na hata vyumba vya Hoteli. Ili kuweza kujiridhisha, na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji muda ili ijiridhishe. Kwa hatua ya awali, iliutaka Uongozi wa Hoteli kuwasilisha mbele ya Kamati, mikataba ya kumbi hizo (na tayari wameshawasilisha).

Pamoja na kuwasilishwa kwa Mikataba hiyo bado Kamati haijridhika na maelezo yaliyomo ndani ya Mikataba hiyo ikiwemo utaratibu wa baadhi ya malipo katika mikataba hiyo kama yalivyo fafanuliwa. Kwa mfano katika Mkataba wa ukodishwaji wa ukumbi wa “Komba Disco’ kuna matumizi ya tsh 20,000,000 kwajilia ya ujenzi wa ukumbi kwa kila mkupuo wa malipo (Installment). Aidha baadhi ya sehemu za Hoteli zimekodishwa kwaajili ya matumizi ya maofisi na vyumba ya kawaida, Kamati inahitaji kupatiwa ufafanuzi wa maeneo yote hayo ikiwemo Mikataba ya ukodishwaji wake , wakodishwaji na kiwango cha pesa zinazoingi kupitia kodi za sehemu hizo. Vile vile ilikujiridhisha mbali na Mikataba hiyo iliyowasilishwaamabyo yote ni ya muda wa mwaka mmoja tu Kamati inataka kupatiwa Mikaba ya mika ya nyuma kwaajili ya ufafanuzi zaidi. Kamati itakutana na Uogozi wa Hoteli kupata ufafanuzi yakinifu juu mambao yanayoleta utata ikiwa ni pamoja na kupatiwa risti za mauzo mbali yanayofanywa hotelini hapo.

Kwa upande mwengine Kamati imefahamu kwamba Uongozi wa Hoteli ya Bwawani hauna Hati miliki ya Hoteli hiyo, jambo linalopelekea, pamoja na mambo mengine kuongezeka kwa vitendo vya uvamizi katika maeneo ya hoteli kwa ujenzi wa maduka na hata makaazi ya watu, wakati huo huo kwakukuwa na jitihada zozote zilizochukuliwa za kupambana na uvamizi huo. Kamati inasikitishwa na hali hii na inaitaka Serikali kusitisha ujenzi huo mara moja.

3.2 KAMISHENI YA UTALII:

Agizo Nam. 1

Kufikiria namna ya kuwashirikisha wananchi kwenye utalii ili wafaidike. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-325).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati ilielezwa kwamba Kamisheni iliandaa mafunzo kwa wajasiriamali 30 wa vijiji vya pwani, aidha mafunzo kama hayo yalitolewa kwa vikundi 4 vya Unguja na Pemba kuhusu mambo yanayohusu utalii. Kwa upande mwengine Kamati imearifiwa kwamba vijana wapatao 69 walipatiwa mafunzo ya "Out reach program" Katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii – Maruhubi, aidha Kamati imeelezwa kwamaba, kwamujbu wa utafiti walioufanya, idadi kubwa ya waliopatiwa mafunzo ya utalii tayari wameajiriwa.

MAONI YA KAMATI:

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Kamisheni ya Utalii kuwasaidia wananchi kunufaika na utalii, hali inaonesha kwamba bado wananchi hawajanufaika ipasavyo na utalii. Aidha wengi katika ya wananchi wa Zanzibar wanaopata ajira katika sekta ya utalii hususan wananchi wa vijijini ni katika ngazi za chini, hivyo Kamisheni na serikali kwa ujumla ni muhimu ikaongeza mikakati kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wananufaika ipasavyo na Sekta hii.

Agizo Nam. 2

Kufikiria namna ya kuisaidia jamii kulinda utamaduni na kufanya tafiti juu ya athari ya utalii na njia ya kupunguza athari hizo. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-325).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imearifiwa kwamba Kamisheni imekuwa ikihamasisha Utamaduni wa Zanzibar kupitia maazimisho ya Siku ya Utalii Duniani kwa kujumuisha michezo mbali mbali. Aidha katika vijiji mbali mbali wananchi wamekuwa wakianzisha 'village tour' ambapo wageni hupata fursa ya kupikiwa vyakula vya kiasili pamoja na kuona ngoma za kiutamaduni.

MAOINI YA KAMATI:
Katika suala la utamaduni, kuna kuutangaza utamaduni wa Zanzibar lakini pia kuzuwia usiharibiwe, kinachoonekana zaidi kwa Kamisheni imejikita katika kuutangaza huku hali ya kimaadili ikionekana kuporomoka siku hadi siku. Hivyo Kamati inaitaka Kamisheni ya Utalli kuweka mikakati imara kuhakikisha wanakabiliana na hali hii.

Agizo Nam.3.
Kutoa taaluma ya kuzuia maambukizi mapya ya Maradhi ya Ukimwi kupitia tafiti zinazofanywa kwenye maeneo ya Utalii. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-325).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamisheni kwa kushirikiana na iliyokuwa Wizara ya Utalii, Biashara na Uekezaji zimefanya semina kumi kwa wadau wa Sekta ya Utalii katika Wilaya zote za Zanzibar ili kuzuia maambukizi mapya, aidha kufuatia mafunzo hayo hoteli mbali mbali zimehamasika kuanzisha upimaji wa hiari.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeitaka kamisheni kuongeza nguvu katika kupambana na maambukizi mapya ya Ukimwi kwani imebainika kwamba Utalii kwa kiasi kikubwa unachangia ongezeko la maambukizi mapya ya Ukimwi.

Agizo Nam. 4.
Zanzibar kufaidika na Utalii wakati wa Mashindano ya kombe la Dunia yaliyofanyika Afrika ya Kusini. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-325).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kwamba wakati wa Kombe la Dunia, Zanzibar ilinufaka kwa kupata ongezeko kubwa la idadi ya watalii ambapo kwa kipindi cha mwezi wa Mei 2010 watalii waliongezeka na kufikia 4,452 ambao ni ongezeko la watalii 795 ukilinganisha na mwaka 2009, na katika kipindi cha mwezi Juni 2010 jumla ya watalii 7,272 waliingia Zanzibar ukilinganisha na watalii 6,514 walioingia mwezu Juni mwaka 2009.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeipongeza Kamisheni kwa hili na pia imeitaka ilichukuwe kama ni funzo kwa hatua za kukuza utalii Zanzibar.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Tatizo la Utalii kutowanufaisha Wananchi wa Zanzibar, bado linaonekana ni sugu pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Kamisheni ya Utalii katika kuwahamasisha wananchi wetu. Aidha, Mapato ya Utalii yanavuja sana Zanzibar. Tatizo hili pamoja na sababu nyengine, pia linasababishwa na kuwekwa kwa Wahasibu na P.O wa kigeni katika Mahoteli ya Kitalii yaliyopo nchini. Kinachoonekana kwa ujumla katika nafasi za juu, wageni ndio wanaoajiriwa na wazalendo hubakishwa kufanya kazi za chini ambazo maslahi yake mara nyingi huwa ni duni. Hili pia hufanywa kwa malengo ya ukwepaji wa kodi ambapo kwa waajiriwa hao kushirikiana na wamiliki wa hoteli, na kutoa taarifa zisizo na usahihi wowote wakati wa ukaguzi.

Pamoja na kuruhusu Utalii, Zanzibar ni nchi yenye utamaduni wake na unapaswa kutunzwa na kuendelezwa. Ni vyema Kamisheni

ikazidi kulitilia nguvu suala hili na kupiga vita aina zote zinazohatarisha kuharibu utamaduni wa Zanzibar.

Kuna mkanganyiko wa ukusanyaji wa mapato ya Utalii. Kodi za aina mbali mbali katika chanzo kimoja cha Utalii zinakusanywa na Kamisheni ya Utalii, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB), Baraza la Mapispaa na hata Taasisi nyengine. Kamati inaitaka Serikali itafute suluhisho la tatizo hili, ili kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na Utalii.

Kamati imefahamishwa kwamba, Shirika la Utalii ni sawa na Makampuni mengine ya Uendeshaji wa Hoteli za Kitalii (Tour Operators) kinachotafautisha ni kwamba, Shirika hili liko chini ya Serikali. Kama ni hivi, bila ya shaka lingepaswa likate leseni ya Utalii katika Kamisheni ya Utalii. Tatizo liliopo, Shirika halikati leseni ya Utalii na kufanya hivi ni kuwapunguzia ukusanyaji wa mapato Kamisheni na pia Serikali.

Licha ya ukweli kwamba Kamisheni ya Utalii ndio yenye dhamana ya kusimamia maendeleo ya Utalii Zanzibar Sekta ambayo ni tegemeo muhimu kwa uchumi wa nchi, bajeti wanapangiwa Kamisheni ya Utalii ni ndogo sana kiasi cha kushindwa kumudu gharama za uendeshaji vizuri jukumu hilo. Hili lingepaswa liangaliwe tena na Serikali ili kuiwezesha Kamisheni kutekeleza vyema majukumu yake.

Aidha, kutokuwa na Akaunti (Account) ya Kamisheni ni tatizo licha ya kuwa sheria Namba 6. 2009 kifungu cha 12 cha sheria hiyo kinaruhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Kamisheni. Ili kuliondosha tatizo hili, Kamati inaitaka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuharakisha upatikanaji wa ‘Account’ hiyo, ili kuiwezesha Kamisheni kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kamati inahisi ipo haja ya kufanyika Ukaguzi Maalum ‘Special Auditing’ kwa sekta ya utalii kuhusu mapato yanayopatikana. Kufanya hivi kutaisaidia Serikali kufahamu mapato halisi yanayokusanywa, na sababu za kuvuja kwa mapato hayo.

3.3 SHIRIKA LA UTALII:

Agizo Nam 1.

Shirika kutafuta Mkaguzi wa ndani ili aweze kupunguza kasoro za fedha zilizojitokeza katika Hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 45.6 (2007/08). (Agizo hili linatokana Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-106).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imearifiwa kwamba kutokana na mjadala wa kuwepo ama kutokuwepo kwa Shirika bado unaendelea Serikalini, Shirika halikuweza kuomba idhini ya kuajiri Mkaguzi wa Ndani na badada yake wanaendelea kumtumia Mkaguzi wa Ndani wa Wizara.

MAONI YA KAMATI:

Kamati inaishauri Serikali ikamilishe Mjadala wa uwepo wa Shirika, ili Shirika kama litaamuliwa kuwepo liweze kujiendesha, ikiwa ni pamoja na kuajiriwa Mkaguzi wa ndani wa Shirika.

Agizo Nam. 2

Shirika kuendelea kufuatilia kesi inayohusiana na deni la Royal Star USD 19,850. (Agizo hili lintokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-106).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati iliarifiwa kwamba Shirika lilimpeleka mwanasheria Ndg. Ali S. Haneni ili kufuatilia kesi hiyo, lakini kwa bahati mbaya mwanasheria huyu amefariki dunia kabla ya kuwasilisha ripoti yake kwa Shirika. Shirika hata hivyo, limeiarifu Kamati kwamba, meli hiyo imeshauzwa na kumilikiwa na mmiliki mwengine. Aidha, Shirika baada ya kupokea taarifa hizi, halikuchukua hatua nyengine zozote kulifuatilia deni hilo.

MAONI YA KAMATI:

Pamoja na jitihada hizo Kamati bado haijaridhika na hatua iliyofikiwa, hivyo imelitaka Shirika kurudi tena kuifuatilia kesi hiyo ili kujuwa hatma ya deni hilo.

Agizo Nam. 3

Kamati iliagiza kufuatiliwa kwa deni la wadaiwa (deptors) wa Shirika Tsh 6,365,000/=. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-106).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imefahamishwa kwamba, deni la Tsh.200,000/- analodaiwa Ndg. Moh'd Juma halijalipwa na Shirika linataka kulifuta baada ya kukaa kwa Bodi ya Shirika ambayo kwa sasa haipo. Aidha, deni la Tsh. 1,100,000/- linalotokana na ukodishwa wa Stare Club, Kamati imepata majibu mawili yenye kutatanisha, kwanza imeambiwa kwamba Mwanasheria wa Shirika baada ya kesi kufunguliwa Mahakamani yeye haikuhudhuria; na jibu jengine ni kwamba, kesi yenyewe haikuwahi kufikishwa Mahakamani kwa sababu Mwanasheria wa Shirika aliacha kazi. Kuhusu deni la Ndg. Azizi la Tsh. 2,300,000/- Shirika linashindwa kulidai deni hilo kwa sababu lililazimika kuvunja mkataba na mdaiwa baada ya kupokea agizo kutoka Serikalini la eneo hilo kupatiwa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

MAONI YA KAMATI:

Kuhusu deni la Tsh. 200,000/, Kamati imebaini kwamba Ndg.Juma analidai Shirika zaidi ya deni analodaiwa kutokana na kulitumikia Shirika bila ya kulipwa. Hivyo, Kamati imeliagiza Shirika lifanye mahesabu ya pesa zinazotokana na posho analodai, ijilipe pesa hizo Tsh. 200,000/- na kama kuna pesa zitakazobakia, wamrejeshee mwenyewe.

Kuhusu deni la Dismass, Kamati imelitaka Shirika kutafuta Mwanasheria mwengine wa kulishauri kuhusiana na deni hilo kisheria. Aidha, kuhusiana na deni la Ndg. Azizi, Kamati haijaridhika na majibu yaliyotolewa na kwa kupitia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji kukutana na aliyekuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Utalii, Biashara na

Uwekezaji pamoja na wahusika wengine kwa ajili ya kupata ufafanuzi zaidi.

Agizo Nam. 4:
Shirika kufuatilia Madeni ya Wadaiwa (Creditors) wa Shirikia. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-106).

MAPITIO YA KAMATI:
Wadai hao wameshalipwa isipokuwa wadai wanne bado hawajalipwa. Jumla ya deni hilo ni Tsh. 8,204,664.15, ambapo Jozani ni Tsh.1,175,664.15; Menai Ths. 460,360.00; Palace Tsh. 3,922,400.00 na Tamarind Tsh.2,646,240.00.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaendelea kuagiza kulipwa kwa madeni hayo. Hata hivyo, inapongeza juhudi zilizochukuliwa kupunguza madeni hayo.

Agizo Nam. 5
Shirika kufanya tathmini mpya ya mali zake na kufunga hesabu zake vizuri na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-107)

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati iliarifiwa kwamba Shirika lilitekeleza agizo hili kwa linafunga hesabu zake na
kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia barua ya
tarehe 29/09/2010 yenye kumbu kumbu namba ZTC/3/9/VOL.1/

MAONI YA KAMATI:
Kamati inapongeza juhudi zilizochukuliwa. Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Kamati inahitaja ya kufahamu zaidi kuhusu ukodishwaji wa Kisiwa cha Changuu. Kuna haja gani ya kuendelea na ukodishwaji wa kisiwa hicho kwa Muwekezaji kwa USD 3500 wakati huo huo kama kingeliachwa kwa Shirika la Utalii, Shirika lingeliweza kukusanya zaidi ya USD 8000 kwa mwezi ikiwa ni pamoja na kumudu gharama za uendeshaji. Kamati inaishauri Serikali kukaa pamoja na Shirika la Utalii ili walitafutie suluhisho suala la ukodishwaji wa Kisiwa cha Changuu.

Kama tulivyoripoti katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuhusu suala la Nyumba zinazomilikiwa kisheria na Shirika la Utalii zilizoko Chwaka zirejeshwe kwa Shirika la Utalii. Kamati imeazimia kukutana na Taasisi husika ili kulifanyia kazi.

4.0 WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO:

Agizo Nam. 1

Wizara kuharakisha malipo ya madeni ambayo Wizara inadaiwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-321).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imearifiwa kwamba Wizara imendelea kulipa madeni hayo, ambapo hadi mwisho wa mwaka huu tayari wamekwishalipa Tsh 15,900,000/=, pia wamekuwa wakitumia baadhi ya fedha kwa ukarabati wa jengo hilo. Hata hivyo, kwa sababu deni hilo linatokana na kodi ya Jengo la Ofisi Kuu ya Wizara, limeongeka na kufikia Ths. 22,699,000/- wakati huo huo Wizara imeshatumia Tsh.13,000,000/- kwa ukarabati wa Jengo hilo. Hata hivyo, Hakuna Mkataba wa ukodishaji wa jengo hilo, wala makubaliano yoyote ya kimaandishi ya ukarabati wake, huku Wizara inatarajia pesa ilizotumia katika ukarabati, Tsh.13,000.000/- ziwe kama ni malipo ya deni la msingi la Tsh. 22,699,000/-.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imeitaka Wizara ikae pamoja na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ili kulizungumzia suala hili na jambo la msingi ni kuwepo Mkataba wa makubaliano hayo. Aidha kamati imeishauri Wizara ifanye utaratibu wa kupata jengo lao kutokana na hasara wanazozipata ikiwa ni pamoja na kodi na gharama za ukarabati wa jengo hilo, lakini pia hata usalama wa jengo hilo ni mdogo kutokana na uchakavu wake.

Agizo Nam. 2

Deni la mdaiwa 'Air Express' la utuaji wa ndege Tsh. 1,161,500/- lifuatiliwe na kuhakikisha linalipwa. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2008/09, uk-37).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati iliarifiwa kwamba kampuni hiyo ilikatisha safari zake bila taarifa yoyote na kuacha deni la tsh 1,166,500/=. Aidha Kamati imearifiwa kwamba idara imefuatilia deni hilo lakini imeshindwa kupata taarifa zozote.

MAONI YA KAMATI:

Kamati haikuridhishwa na majibu hayo ambayo pia yalielezwa kwa Kamati ya mwaka 2008/09 na inahisi hakukuwa na hatua madhubuti katika kulifuatilia deni hili na imeitaka Idara ifuatile Kampuni hii katika Afisi ya Mrajisi ili kujuwa uwepo wake. Aidha Kamati inaishauri serikali, Kampuni yoyote itakayosajiliwa kufanya kazi Zanzibar lazima iwe inadhibitiwa na pia ichukuliwe dhamana juu ya matatizo yoyote yatakayojitokeza.

Agizo Nam. 3

Wizara ipeleke nyaraka za taarifa za uingizaji wa fedha kutoka Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuzipitia. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk- 88).

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo hili halijatekelezwa. Hata hivyo, nyaraka hizo zipo kopi na 'Original' zimekosekana na wala hazijakaguliwa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeitaka Wizara iziwasilishe nyaraka hizo kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ili azikague na pia Kamati iarifiwe juu ya hatua hiyo. Kamati tayari imepokea barua ya tarehe 10 Machi, 2011 yenye kumbu kumbu namba MICZ/B.90/C.1/Vol.X111/154 ya Wizara kuiandikia Afisi ya Mdhibiti ili akague. Hata hivyo, bado Kamati inasisitiza kupewa taarifa ya ukaguzi huo.

Agizo Nam. 4
Wizara iiwezeshe Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za ndani (Audit Committee) na Bodi ya Zabuni ya Wizara (Idara ya Mipango na Uendeshaji), ili ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk- 89).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati iliarifiwa kwamba Wizara imeimarisha ufanisi wa Kamati na Bodi hiyo na inafanya vikao mara kwa mara kujadili mambo mbali mbali ikiwa ni sehemu ya majukumu ya Bodi hiyo. Kwa wastani, Audit Committee imeshafanya vikao 10 na Bodi ya Zabuni imeshafanya vikao 15 kwa mwaka 2009/10 na 2010/11.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeitaka Wizara ipatie Kumbukumbu za vikao hivyo iliijiridhishe zaidi.

Agizo Nam. 5
Wizara iangalie upya kodi za utuaji ndege, Uwanja wa Ndege wa Pemba na kuangalia upya Miradi inayohusika na uboreshaji wa huduma za uwanja huo ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa taa wakati wa usiku . (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk- 89.)

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imearifiwa kwamba viwango vya kodi ya utuaji na uegeshaji wa ndege hutangazwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania(TCAA) kwa kushirikiana na Mamlaka husika kwa mujibu wa hadhi ya kiwanja chenyewe, na hutolewa katika kitabu kwa ajili ya matumizi ya wadau wote wa viwanja vya ndege kitaifa na kimataifa. Aidha kamati imearifiwa kwamba Idara imewasiliana na ADB kuomba ufadhili wa uboreshaji wa uwanja na pia wamewasiliana na wataalamu kutoka Afrika Kusini lakini bado hawajapata fedha kwa utekelezaji wa kazi hiyo, pia Kamati imearifiwa kazi ya kujenga uzio imeshaanza.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imeitaka Wizara kulitilia nguvu zaidi suali la uboreshaji wa kiwanja hicho ili kiweze kutoa hadudi zilizo bora.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Kamati imetaka kufahamu taratibu zilizotumika katika ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Abeid Aman Karume International Airport of Zanzibar), ikiwa ni pamoja na kufanya ziara ya kiwanja hicho. Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inahitaji kulifuatilia suala hili. Suala hili limezuwa utata kwa vile ujenzi huo ulitolewa taarifa kuwa ulijengwa kwa fedha zilizobakia kutoka mkopo wa Banki ya Dunia.

Kamati imefahamishwa kwamba Wizara inakusudia kuhamia Ofisi ya Bohari Kuu ili kupunguza mzigo na athari za kuanguka kwa Jengo wanalolitumia sasa. Kamati baada ya kupokea taarifa hii na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha, 2005 inahitaji ufafanuzi yakinifu kuhusu ukarabati huo ikiwa ni pamoja na vyanzo vya fedha zilizotumika katika ukarabati wake na kutembelea Ofisi hiyo. Kwa vile fdha hizo zilizotumika Tsh 94 milioni kufanyia ukarabati huo ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa Afisi mpya.

Kuhusu Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar, Kamati kwa masikitiko imepokea taarifa za kukosekana maji hasa vyooni, kukithiri kwa wizi katika sehemu ya Mashine za usalama na kuitaka Wizara ifuatilie ukweli wake na warekebishe kasoro hizo.

4.1 IDARA YA ANGA:

Agizo Nam. 1

Idara kufuatilia deni la asilimia 10% lililobakia katika deni la msingi la Tsh. 290,799,944/ na USD 23,028, linalohusiana na utuaji wa ndege kutoka mashirika mbali mbali. Aidha Kamati pia iliitaka kujuwa kwa namna gani Idara imeweza kusimamia madeni hayo tokea mwaka 2008 hadi leo. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-89).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imearifiwa kwamba deni lilobakia ni la Shirika la ndege la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (Air Tanzania) amabalo ni Tsh.140,035,896, deni hilo hivi sasa limefikia Tsh. 241,141,778/- Shirika lilikumbusha kwa barua ya tarehe 24 February 2010 yenye kumbu kumbu namba, DA/AM/ZIA/UT/001/15/95 na kujibiwa na Meneja wa Kituo, Dar es Salaam kwa barua ya tarehe 28/7/2010 kuomba kuruhusiwa kupatiwa huduma za ndege pamoja na kushindwa kulipa deni hilo. Hata hivyo, Idara ilichukua hatua ya kumuandikia barua nyengine ya tarehe 18/08/2010 yenye kumbu kumbu namba, DA/AM/ZIA/UT/001/15/109 kwa Meneja Mkaazi, Shirika la Ndege, Air Tanzania (ATCL), tawi la Zanzibar kuzitaka ndege hizo zilipie baada ya kutuwa tu.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imeridhishwa na jitihada za Wizara lakini pia imeitaka Wizara kuendelea kulifuatatilia deni hilo na kuijuilisha Kamati kwa kila hatua itakayochukua.

4.2 SHIRIKA LA BANDARI:

Agizo Nam. 1

Shirika kuanzisha Bodi ya Wakurugenzi inayopaswa kutoa idhini ya matumizi na taratibu za Shirika, ili kuharakisha utekelezaji wa Miradi ya Shirika. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-49).

MAPITIO YA KAMATI:
Bodi hiyo sasa ipo na inategemea kumaliza muda wake mwaka huu. Kuwepo kwa Bodi hiyo, kulisaidia kurekebisha kasoro mbali mbali zilizokuwepo wakati huo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeridhika na kupongeza jitihada hizo za Shirika.

Agizo Nam. 2
Shirika kufanya Master plan katika bandari zake za Pemba ili kuweza kujua mipaka ya maeneo yake na kudhibiti ujenzi holela katika maeneo ya Bandari. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk 150).

MAPITIO YA KAMATI:
Ili Shirika liweze kutekeleza agizo hili, jambo la mwanzo muhimu ni kupatikana kwa Hati Miliki ya Maeneo ya Bandari. Kamati imeelezwa kwamba tayari Shirika limepata Hati miliki ya Mnara wa Kigomasha pekee na maeneo yote yaliyobakia yameshapimwa na kusubiri zipatikane hati hizo. Shirika linaomba kupatiwa Hati hizo ili liweze kufanya ‘Master Plan’ na kuboresha shughuli zake. Shirika limeifahamisha Kamati kwamba limeshapeleka maombi na kukamilisha taratibu zote zinazohusika, ila bado halijapatiwa Hati Miliki za maeneo hayo.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na juhudi zilizochukuliwa, Kamati imetaka kupatiwa ushahidi wake kwa maandishi ili iweze kujiridhisha. Hata hivyo, tatizo la kukosekana na kucheleshwa upatikanaji kwa Hati Miliki ni kubwa zaidi kwa Taasisi za Serikali. Kamati inashanganzwa na hali hii na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za

mwaka 2005, Kamati inahitaji kukutana na Wizara inayohusika na Ardhi ili iweze kupata ufafanuzi.

Agizo Nam.3

Uongozi wa Shirika la Bandari (Pemba) kufanya juhudi za makusudi za kuondosha ajira za watoto katika bandari hiyo. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-150).

MAPITIO YA KAMATI:

Shirika kwa kushirikiana na vyombo vya Dola, limejitahidi kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo hili.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imepongeza juhudi zilizochukuliwa na kulitaka kuendelea kulifanyia kazi zaidi ili kuliondosha kabisa.

Agizo Nam. 4

Shirika kutafuta haraka vifaa vya kupakulia mizigo katika bandari ya Malindi. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2008/09, uk-35).

MAPITIO YA KAMATI:

Juhudi za kulimaliza tatizo hili zinaendelea na Shirika linatarajia kulimaza kabisa mwaka 2014 kwa vifaa hivyo kupatikana kwa bandari zote, Unguja na Pemba. Hata hivyo, tatizo la ukosefu wa fedha linakwamisha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa vifaa hivyo kwa wakati.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imezidi kulisisitiza suala la vifaa ili kuongeza ufanisi wa bandari hasa ikizingaitwa kwamba ni sehemu muhimu kwa mustakabali wa uchumi wa Taifa

Agizo Nam.

Kuharakishwa mpango wa kujenga gati nyengine ili kwenda sambamba na ushindani wa biashara na nchi jirani. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2008/2009).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati mimearifiwa kwamba Shirika limo katika mpango huo, tayari wamefanya mazungumzo na wataalamu wa kichina na kufanya stadi ya awali (Feasibility Study) ili iliifikishe Serikalini na baadae kuwasilishwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuthibishwa na hatimae kuombewa mkopo wa USD 300,000,000 kutoka "Exim Bank" ya Kichina, lakini bado hawaja pata fedha za kugharamia mradi huo**.**

MAONI YA KAMATI:

Kamati inaridhishwa na jitihada hizo na inaiomba Serikali kusaidia suala hili kwani kukamilika kwa mradi huu ni hatua muhimu sana kwa uchumi wa nchi.

Agizo Nam. 6

Kamati iliuagiza uongozi wa Shirika kupata 'manifest' ya meli zilizosafirisha bidhaa

Bandarini Zanzibar.

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati ilielezwa kwamba, tatizo la kukosekana kwa 'manifest' hizo limesharekebishwa na sasa zinapatikana kwa wakati

MAONI YA KAMATI:

Kamatii imepongeza juhudi hizo.

4.3 SHIRIKA LA MELI:

Agizo Nam. 1

Shirika kuchukua hatua za kupunguza gharama za utawala na kuwa wabunifu kwa kutafuta vyanzo vya mapato kwa lengo la kuinua uwezo wa Shirika. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-145).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imepewa maelezo yale yale ya miaka mitatu iliyopita kwamba, ili kupunguza gharama na kuinuwa uwezo wa Shirka, ni lazima lipunguze wafanyakazi kwa kuwastaafisha baadhi, pamoja na kuzuwia ajira mpya, ispokuwa kwa kada ya wahandisi tu (engineers), jambo ambalo linashindikana kutokana na ukosefu wa fedha na uwezo mdogo wa Shirika.

MAONI YA KAMATI:
Kimsingi Kamati imeyapokea majibu hayo, tatizo kama hili pia linayakabili Mashirika mengi ya Serikali. Katika njia za kulitafutia ufumbuzi, Kamati ina azma ya kukutana na Mashirika yote ya Serikali ili kujaribu kulitafutia ufumbuzi tatizo hili.

Agizo Nam.2
Shirika kuchukua hatua, na kulipeleka Serikalini tatizo la meli chakavu ili lipate ufumbuzi, ikiwa ni pamoja na kutafuta meli nyengine za kisasa zitakazomudu hali ya ushindani wa biashara. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-345).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kwamba Shirika limetekeleza agizo la kulipeleka serikalini tatizo la meli chakavu na kuishauri Seriakali kuzi “phase out” ambapo Serikali imechukuwa hatua ya kuiuza meli ya M.V Mapinduzi kwa Kampuni ya ‘Badr East Africa Enterprises Ltd(Dsm)’.
Kuhusu ununuzi wa meli mpya ya Serikali, Kamati imefahamishwa kwamba Shirika ilichukua hatua ya kutafuta meli hiyo, hata hivyo, baada ya kufikisha wazo hili Serikalini kwa kupata udhamini, Serikali, kupitia barua ya tarehe 13 Januari, 2011 yenye kumbu kumbu WMU/17/VOL.1/1 iliagiza ununuzi wa meli hiyo usite mara moja.

MAONI YA KAMATI:

Kamati inipongeza hatua za uuzaji wa meli chakavu. Kuhusu agizo la Serikali kulikataza Shirika kununua meli hiyo, haikuliridhisha Kamati na kuifanya Kamati iwaite Katibu Mkuu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Meneja Mkuu, Shirika la Meli na Uwakala pamoja na watendaji wao watakaoweza kuisaidia Kamati kupata ufafanuzi wa kina. Hata hivyo, Kamati pia ilimwita Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kupitia barua ya tarehe 04/03/2011 yenye kumbu kumbu namba BLW/K.10/2/33, lakini kwa masikitiko makubwa Mhe. Waziri hakuweza kuhudhuria bila ya kutoa taarifa yoyote. Kamati inasikitishwa na hali hii na kuwataka Mawaziri waheshimu wito wa Kamati.

Pamoja na majibu yaliyotolewa mbele ya Kikao hicho, Kamati haikupata ufafanuzi yakinifu na hivyo, kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha, 2005 inahitaji kupata muda ziada wa kulifanyia kazi suala hili. Hivyo, kwa hatua za awali, Kamati imewataka Meneja Mkuu Shirika la Meli, Makatibu Wakuu wa Wizara mbili hizi, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kukutana pamoja na baadae kikao kama kilichoitwa hapo kabla kiitishwe na Shirika la Meli na Uwakala ili Kamati ipate muda wa kulifanyia kazi tena.

Agizo Nam. 3

Shirika kuchukua juhudi za makusudi kulipa madeni yake ili liweze kuwa na “current ratio” nzuri. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-145).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imeelezwa kwamba Shirika limejitahidi kuweza kusawazisha madeni yake yote ya zamani amabayo yalikuwa yanadaiwa kwa ajili ya matengenezo ya meli zake.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imepongeza na kuziunga mkono jitihada hizo za Shirika.

5.0 OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI.

Agizo Nam.1

Ofisi kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuzifanyia ukaguzi taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati kuhusu malipo yasiyo na stakabadi. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-318).

MAPITIO YA KAMATI:

Wakati wa Kamati wa Kamati ilielezwa kwamba suala hilo limeshafanyiwa kazi. Hata hivyo, Kamati ilipotaka kupatiwa uthibisho wa maandishi kuhuu utekelezaji wa agizo, Ofisi haikuwa na jawabu na kuahidi kuziwasilisha kwa Mdhibiti haraka iwezekanavyo. Aidha, kwa kupitia barua yao ya tarehe 03/03/2011 yenye kumbu kumbu namba AR/IKL/B.90/5.VOL III/84 Kamati imepokea taarifa kwamba Ofisi imeviwasilisha vielelezo hivyo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili avikague.

MAONI YA KAMATI:

Kamati inaitaka Ofisi, baada ya ukaguzi huo itoe taarifa kwa Kamati.

5.1 KUHUSU HALMASHAURI ZA WILAYA:

Agizo Nam. 1

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufanyika mabadiliko katika mfumo mzima wa Serikali za Mitaa kwa lengo la kuzijengea uwezo na kuzipa nguvu za kukusanya mapato. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-174).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imeelezwa kwamba jitihada mbali mbali zinafanyika katika kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa. Ofisi imeufanyia stadi ya awali (feasibility study) mfumo mzima kuona jinsi gani wataweza kuziendesha kwa ufanisi pia wamewapeleka wafanyakazi kupata mafunzo ya muda mfupi. Aidha katika kikao cha Oktoba au Januari cha Baraza la Wawakilishi wanatarajia kuleta Sera ya Serikali za Mitaa, vile vile katika mabadiliko ya taasisi za umma (Public Sector

Reform) imo sehemu inazungumzia Serikali za Mitaa na hivyo, wanatarajia itasaidia kueka mfumo bora wa uendeshaji wa Serikali za Mitaa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeagiza mabadiliko hayo yawekewe muda na mikakati maalum na yalenge kuzijengea uwezo kwani limekuwa ni tatizo la muda mrefu sasa kwa Serikali za Mitaa kutokuwa na ufanisi.

Agizo Nam. 2
Kamati iliagiza kuchukuliwa hatua za haraka za kuwapatia mafunzo maofisa wote wanaoshughulika na uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu za Halmashauri. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007,2008, uk-174).

MAPITIO YA KAMATI
Kamati imearifiwa kwamba Wizara imechukuwa hatua ya kuwapatia mafunzo wafanya kazi mbali mbali, aidha Mhasibu Mkuu wa Serikali ameweka utaratibu wa kuweka wakaguzi watano wandani kwa kila Wizara.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kuwa Kamati ilipata maelezo haya kwa njia ya mazungumzo ya mdomo tu, imeiagiza Ofisi kuipatia Kamati mchanganuo wa mafunzo hayo kwa mandishi kwa kila wilaya ili iweze kujiridhisha. Mpaka tunaandika ripoti hii, Kamati bado haijapokea taarifa hiyo.

5.2 HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIB:

Agizo la ulipaji wa Deni la Tsh. 100,000/- alilokopeshwa Ndg. Mohammed A. Ahmeid (linatokana na Ripoti ya Kamati, 2008/09, uk-44 kama ilivyoripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupita Hoja Nam. 20.6.4 ya mwaka 2004/05.)

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati imefahamishwa kwamba, mdaiwa huyo tayari ameshalipa pesa hizo kupitia Risiti No. 096665 ya terehe 14/01/2009, na fedha hizo zimeshapelekwa Benki kama zilivyo taratibu, pia imeshakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

5.3 CHUO CHA MAFUNZO:

Agizo.
Uongozi wa Chuo kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa taarifa zilizokuwa zimekosekana wakati wa ukaguzi ambazo ziliwasilishwa mbele ya Kamati. (Agizo hili linatokana Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-319.)

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati iliarifiwa kwamba Uongozi wa Chuo ulizikabidhi taarifa hizo kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ ambaye yeye alipaswa aziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili azikague.Kamati imethibitisha barua hiyo na kujiridhisha.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepogeza jitihada zilizochukuliwa na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, inapendekeza hoja hii ifutwe.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Kuna matatizo mengi na makubwa ya wingi na mlundikano wa Rumande. Kamati inashauri Wizara ifanye utaratibu wa kujenga Chuo chengine ili kuondosha kasoro hizi pamoja na kuwa na cha kisasa chenye kwenda sambamba na mabadiliko ya wakati.

5.4 KIKOSI CHA VALANTIA:

Agizo.

Kikosi kutafuta vielelezo zaidi vya kuhalalisha malipo yaliyofanyika kwa 'Mtoni Motors Agency', kupitia Hund No. 284392, kwa thamani ya Tsh. 12,733,450. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-87).

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati iliarifiwa Kikosi kilinunua magari yenye thamanai ya zaidi ya Tsh. 24,000,000 lakini fedha ambazo zilikosekana stakabadhi zake, ni Tsh 12,733,450 amabazo kwa wakati huo hazikuambatanishwa, lakini baadae stakabadhi zilipatikana na kuthibitishwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imepogeza jitihada zilizochukuliwa na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, inapendekeza hoja hii ifutwe.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Kamati inahitaji kufahamu Utaratibu wa ujenzi wa Makao Makuu ya Kikosi-

Mtoni, ili kujiridhisha kama fedha zilizotumika zinawiyana na thamani halisi ya

Fedha na taratibu nyengine za kisheria.

Kamati inaishauri Kikosi kutafuta vyanzo vya mapato kupitia ujenzi. Kwa kuwa wanao mafundi il isipokuwa bado hawajapata ujuzi na uzoefu mkubwa, Kamati inashauri wawaendeleze katika elimu za ufundi ili waweze kuwatumia ipasavyo.

Kamati imefahamu kwamba, Fedha zinazotengwa kwa ajili ya Ukimwi hazitumiki ipasavyo. Kwa mfano kikosi huzitumia kwa matumizi mengine. Kamati inaishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu kuzikagua ipasavyo fedha hizi ili kuona kama zinatumika kama ilivyokusudiwa.

6.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Agizo Nam.1
Wizara kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua vifaa zilivyoingizwa katika daftari la vifaa. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-334).

MAPITIO YA KAMATI:
Vifaa hivyo vimekaguliwa mbele ya Kamati, ispokuwa baadhi vocha za kuhalalisha manunuzi ya vifaa hivyo hazikuonekana kutokana na Wizara kuhama jingo la zamani la ofisi.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imelikagua daftari la vifaa hivyo, pamoja na kasoro zilizojitokeza imeridhika uhalali wa unuzi wa vifaa hivyo. Aidha, kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, inapendeleza hoja hii ifutwe.

Agizo Nam.2
Wizara kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali stakabadhi zilizokosekana wakati wa ukaguzi na kupatikana wakati wa Kamati. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-334).

MAPITIO YA KAMATI:
Risiti zilizohitajika ni 5, 3 kati ya hizo zimekosekana mpaka wakati wa Kamati. Wizara imethibitisha kupotea kwake kutokana na sababu ya kuhama jingo la ofisi.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na kasoro zilizojitokeza, kutokana na sababu ya kuhama jingo na kwa kuwa hoja hii ni ya muda mrefu, Kamati kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha kanuni za Fedha, 2005, inapendekeza hoja hii ifutwe.

Agizo Nam.3

Kukiendeleza Chuo cha Ufundi, Kengeja ili kuendane na hadhi ya Chuo cha Ufundi kama kilivyokusudiwa. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-113).

MAPITIO YA KAMATI
Wizara imeanza kuchukua hatua ya utekelezaji wa agizo hili kwa kuanzisha mradi wa Uimarishaji wa Vyuo vya Ufundi, Karume na Kengeja, aidha wamenunua vifaa vya kufundishia sayansi na ufundi kupitia mradi huo na kupelekwa Kengeja. Hata hivyo, wanakabiliwa na upungufu wa walimu wa sayansi na ufundi tatizo ambalo pia linazikabili skuli za kawaida.

MAONI YA KAMATI
Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha kanuni za Fedha za mwaka 2005, suala hili linahitaji kufanyiwa kazi zaidi, na hivyo, Kamati inahitaji kutembelea Chuo hicho ili ijiridhishe.

7.0 WIZARA YA AFYA:

Agizo Nam.1:
Wizara kuendelea na juhudi za kutafuta msaada wa ujenzi wa wodi ya watoto kwenye Hospitali ya Abdalla Mzee. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-330).

MAPITIO YA KAMATI:
Utekelezaji wa agizo hili bado haujaanza. Hata hivyo, Wizara inatarajia kuanza utekelezaji wake kupita Mradi mpya wa ‘Zanzibar Primary Health Project’ utakaofadhiliwa na ‘African Development Bank’ (ADB).

MAONI YA KAMATI:
Kamati imejenga matumaini ya utekelezaji wa agizo hili kupitia Mradi huo. Aidha, Kamati inashauri agizo hili lifanyiwe kazi na Mradi usimamiwe ipasavyo kwa maendeleo ya Hospitali hiyo.

Agizo Nam. 2:
Wizara kuvitafuta viambatanisho vya malipo ya kusafirishia wagonjwa nje ya nchi na baadae kuviwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kukaguliwa na

kujuilishwa kwa Kamati kuhusu utekelezaji huo. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-330).

MAPITIO YA KAMATI:

Wizara imeshindwa kuvipata vielelezo hivyo kutokana na sababu zifuatazo:

- Utekelezaji wa agizo la Kamati zilizopita la kutoa tangazo na kuwaita wahusika kupitia vyombo vya habari ni gumu kwa sababu wahusika wengine wameshafariki dunia hivyo itapelekea wafiwa kukumbuka machungu ya vifo vya watu wao.
- Fedha zinazotolewa kwa matibabu hayo ni kidogo na mgonjwa huahidi ataongezea mwenyewe lakini baadae harejeshi vielelezo vyovyote.
- Wagonjwa wengine hufariki dunia kabla au baada ya matibabu, hivyo inapelekea kukosekana kwa vielelezo husika.
- Wagonjwa wengi hufuatana na jamaa au watoto wao na sio wafanyakazi wa Wizara (Staff Nurse) kama ulivyo utaratibu.

MAONI YA KAMATI:

Pamoja na kasoro zilizopo, Kamati inaagiza utafutwe utaratibu wa kupatikana kwa vielelezo hivyo kwa ajili ya kuthibitisha uhalali wa matumizi ya fedha hizo. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuanzia sasa itafute utaratibu utakaohakikisha vielelezo hivyo vinapatikana ili kuweka utaratbu mzuri wa fedha za umma.

Agizo Nam. 3:

Wizara iwalipe mishahara yao wafanyakazi walioathirika na wizi wa mishahara uliotokea mwaka 2008, katika Wizara ya Afya, Pemba. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-108).

MAPITIO YA KAMATI:

Wizara mpaka wakati wa kazi za Kamati, imeshawalipa wafanyakazi wanne (4) tu, kati ya wafanyakazi 62 walioathirika na wizi huo. Hata hivyo, Wizara imeahidi mbele ya Kamati kwamba itawalipa wafanyakazi waliobakia kabla ya kikao cha Bajeti ya Serikali, 2011/2012.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imesisitiza kutekelezwa kwa agizo hilo kama Wizara ilivyoahidi. Kamati pia iliiagiza Wizara kuwasiliana na Ofisi ya Raisi, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo juu ya suala hilo

ambapo Wizara ya Afya kupitia barua ya tarehe 09/03/2011 yenye kumbu kumbu namba WA/F.10/C.5 imetekeleza agizo hilo.

8.0 OFISI YA RAIS, FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO:

Agizo Nam.1:
Wizara kukaa pamoja na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuyaangalia na kuyapatia ufumbuzi madeni sugu na yasiyolipika ya Wizara, Idara na Taasisi mbali mbali za Serikali. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-108)

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo hili limetekelezwa kwa Wizara na Afisi ya Mdhibiti kukaa pamoja na kutoa mchanganuo wa kiwango cha fedha kinachodaiwa, kilicholipwa na kilichobaki pia unaonesha anaedai na anaedaiwa.

Muongozo wa sheria uliotumika ni kupitia Kifungu cha 20 (1) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, ambapo madeni hayo yanawajibika kuwasilishwa kwenye Kamati kwa kuhakikiwa na baadae kuingizwa kwenye hesabu za Serikali kama ni hasara. Baada ya kuingizwa kwenye hesabu za Serikali kama ni hasara, zitawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi ambalo linaweza kumruhusu Waziri anaehusika na mambo ya fedha kulifuta deni hilo au kwa kiwango ambacho Baraza litaruhusu.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepokea uchambuzi huo wa madeni kutoka Wizarani kupitia barua ya tarehe 10/03/2011 yenye kumbu kumbu namba OR/FUMM/N10/03VOL5/96 na inatarajia kukaa kwa hatua zinazofuata.

Agizo Nam.2:
Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya zipewe asilimia Fulani ya mapato ya vianzio vilivyomo kwenye maeneo yao ya kazi. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-318).

MAPITIO YA KAMATI:

Marekebisho yanayohitajika katika agizo hili yanategemea kupata ufumbuzi kupitia Marekebisho "Reform" ya Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji inayoendelea kufanyiwa kazi Serikalini.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inasubiri 'Reform' hiyo na kuitaka Serikali ikamilishe ili iwasilishwe Barazani na hatimae kufanyiwa kazi.

Agizo Nam.3
Wizara kulipa malipo yote ya Wastaafu kwenye kituo kimoja, badala ya kulipa kwenye vituo viwili, yaani Hazina na ZSSF kwa lengo la kupunguza usumbufu wanaoupata wastaafu hao. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-344).

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo hili limetekelezwa. Kwa sasa wastaafu wote hupokelea pencheni zao ZSSF. Hazina kwa kila mwezi huandika hundi na kuilipa ZSSF ili kuwalipa wastaafu pencheni zao. Wastaafu wanaopokea Hazina ni wale tu ambao hawamo katika mfuko wa ZSSF.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza utekelezaji wa agizo hili.

Agizo Nam. 4.
Ofisi Kulipa deni la Tsh.13,000,000/- linalotokana na mashamba ya Wakfu yaliyochukuliwa na Serikali ambayo bado hayajalipwa fidia. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-318).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba deni hili tayari limeshalipwa.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, ili Kamati ijiridhishe imeagiza ipatiwe uthibitisho wa malipo hayo. Mpaka tunaandika ripoti hii, bado Kamati haijapatiwa uthibitisho huo.

Agizo Nam. 5:
Kuangalia malalamiko ya wafanyakazi waliostaafishwa PBZ, ambao walilalamika kwamba zoezi la kustaafishwa kwao halikufuata taratibu za kisheria. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-363-364).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba, Baada ya wastaafu hawa kutoridhika, walilipeleka dai hili Mahakamani ambapo Mahkama iliamua, kuwa utaratibu wa kuwastaafisha haukuwa na dosari na hivyo hawana madai ya ziada.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, Kamati imeagiza kupatiwa nakla ya Hukumu hiyo, ili iipitie na kujiridhisha. Mpaka tunaandika ripoti hii, nakla hiyo ya Hukumu bado haijapatikana.

Agizo Nam. 6:
Ofisi kuzisaidia Halmashauri kuwa na Wahasibu (na watendaji wengine wa masuala ya fedha) waliosomea wenye ujuzi na mambo ya fedha. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-107/108).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati ilifahamishwa kwamba, hatua za kuwapeleka Wahasibu wenye sifa zimekamilika na Ofisi ilitaraji kuanza zoezi hili siku ya Jumatatu ya tarehe 14/03/2011.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imefurahishwa na taarifa hiyo, ila inasisitiza kwamba baada ya zoezi hilo la kuwapeleka Wahasibu wenye sifa, Ofisi iangalie pia utekelezaji wa agizo hili kwa upande wa watendaji wengine wa masuala ya fedha.

Agizo Nam. 7
Ofisi irekebishe kasoro za uingiaji wa fedha “Other Charges (O/C)” kwa upande wa Pemba. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-109.)

MAPITIO YA KAMATI:
Kasoro hizi sasa zimerekebishwa, hivyo, fedha hizo ambazo mgao wake unakuwa tayari umo kwenye “Cash Flow” iliyowasilishwa na Wizara husika, hivi sasa zinapelekwa Pemba moja kwa moja na kutolewa taarifa zake kwa Accounting Officer anaehusika.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inapongeza juhudi hizi za kuondosha kasoro hizo.

Agizo Nam. 8:

Ofisi ihakikishe kwamba Wakaguzi wa Ndani wa Wizara na Taasisi nyengine za Serikali, wanapewa fursa ya kutekeleza majukumu yao ipasavyo, kama inavyofanywa kwa Wahasibu. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-108).

MAPITIO YA KAMATI:
Utekelezaji wa agizo hili ni pamoja na wakaguzi hawa kupatiwa nafasi za masomo ya muda mfupi na mrefu na kujengewa mazingira bora ya kazi. Fursa walizopewa ni pamoja na kuandaa mipango ya kazi ya mwaka na kuthibitishwa na Afisa Mhasibu na Kamati ya Mkaguzi, kutoa taarifa ya ukaguzi na kuziwasilisha kwa Afisa Mhasibu, Mhdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, Kamati inaipongeza Ofisi kuchukua hatua hii lakini inaitaka iendelee na jitihada hizi.

Agizo Nam. 9
Ofisi kulipa madeni ya watu binafsi waliokuwa wakutoa huduma mbali mbali katika hospitali za Pemba. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-109).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba, suala la madeni ya Wazabuni linaendelea kuwa changamoto kubwa kwa Serikali. Hata hivyo, Serikali ina azma ya kulipa madeni hayo kwa haraka zaidi mwaka huu wa fedha (2011/2012).

MAONI YA KAMATI:
Kamati inasisitiza madeni hayo yalipwe na ipatiwe maendeleo ya malipo hayo.

Agizo Nam. 10
Ofisi kutafuta suluhisho la tatizo la baadhi ya Taasisi za Serikali kukosa mifumo bora ya kiuhasibu, mfano wa kuzingatiwa ni Shirika la Umeme, Tawi la Pemba (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-108).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba, Sheria za Fedha za Umma na Kanuni zake zinatoa muongozo wa kiuhasibu. Wizara inayohusiana na Fedha nayo hutoa miongozo, maagizo na hata matoleo mbali

mbali kwa Wahasibu, aidha kila Shirika linafursa ya kutunga Kanuni za ndani kwa lengo la kupatikana ufanisi. Kuhusu Mfano huo wa Shirika la Umeme, Ofisi ilikiri kuwa lilikuwa ni tatizo na wao waliliandikia barua kulitaka lirekebishe kasoro hizo.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, Kamati inahitaji kulifuatilia hili Shirika la Umeme, Pemba ili kuona kama tayari wamesharikebisha.

Agizo Nam.11
Ofisi kukiongezea nguvu Chuo ch Uongozi wa Fedha. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08).

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo linaendelea kutekelezwa. Ofisi imeongeza huduma ya majengo ya Chuo na Chuo kimeweza kuanzisha kutoa taaluma mpya mpya ikiwa ni pamoja na "Procurement", kuajiri walimu wenye sifa zinazohitajika na kuendelea kuwapatia elimu ya ziada walimu hao.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inasisitiza juhudi hizo ziendelee kuchukuliwa.

Agizo Nam. 12.
Ofisi kukamilisha Mfumo mmoja wa kuweka kumbu kumbu mali za Serikali "Assets Registrer"

MAPITIO YA KAMATI:
Ofisi imefahamisha kwamba tayari wameshakamilisha Mfumo huo na wameshatoa kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali na Mashirika, isipokuwa kwa Wizara 3 mpya ziliongezeka katika Awamu hii. aidha, Ofisi pia imetoa taaluma ya matumizi ya mfumo huo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeipokea taarifa hii na kuzitaka taasisi zote husika zitumie mfumo huu na ile hoja ya kusubiri muongozo huo sasa haina msingi tena. Aidha, Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma ihakikishe Taasisi zinazohusika zinautumia mfumo huo.

Agizo Nam. 13:
Aliyekuwa Mhasibu, Shirika la Huduma za Maktaba alieripotiwa kukiuka Sheria na Kanuni za Fedha achukuliwe hatua za Kisheria.(Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2008/09, uk-41).

MAPITIO YA KAMATI:
Suala hili kwa mara ya mwisho limekabidhiwa vyombo vya Dola kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, isipokuwa taarifa zilizopo Mtuhumiwa amekimbia na hajuilikai alipo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaitaka Ofisi kuendelea na hatua.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Kuna suala la Uhaulishaji "Reallocation" kwa takriban Taasisi zote za Serikali. Kamati imefahamishwa kwamba hali hii inatokana na umasikini unaoikabili nchi yetu kunakowapelekea Wahasibu wa Taasisi hizi kufanya Uhaulishaji mara kwa mara.

Kamati imegundua kutowekwa vipaumbele vya matumizi muhimu kutokana na Ukomo wa Bajeti "Ceiling" ya matumizi husika. Pamoja na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, kuna haja ya kupatikana uelewa wake kwa Wahasibu wa Taasisi hizo, na hivyo, Kamati inaitaka Ofisi ihakikishe kwamba, muongozo sahihi unatolewa kwa Taasisi hizo.

Kuhusu uanzishaji wa Sera ya Kodi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inaendelea kulifanyia kazi kwa kuangalia kwa kina haja ya uwepo wa Sera hiyo ama kutokuwepo kwake.

8.1 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (ZSSF):

Agizo Nam. 1:
Mfuko kutoa elimu kwa waajiriwa wa Taasisi mbali mbali ili kuongeza wananchama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-164).

MAPITIO YA KAMATI:
Uongozi wa Mfuko unaendelea kutekeleza agizo hili kwa sababu agizo lenyewe ni endelevu. Katika utekelezaji wake, Uongozi umeunda timu maalum ya kutoa elimu kwa waajiri na waajiriwa na kuongeza idadi ya makusanyo hadi kufikia Bilioni 3.7, sawa na asilimia 104.5 ya lengo lililowekwa. Hata hivyo, changamoto

wanazozipata ni pamoja na wateja wengi wanataka kufaidika na malipo ya muda mfupi na hili linahitaji marekebisho ya Sheria ya Mfuko.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza juhudi zinazochukuliwa na kuutaka Uongozi uendelee na kutoa elimu hiyo pamoja na kuifanyia marekebisho Sheria ya Mfuko ili iendane na wakati.

Agizo Nam. 2:
Kutafutwa na hatimae kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, stakabadhi zilizokosekana wakati wa ukaguzi na kuwasilishwa mbele ya Kamati. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-164).

MAPITIO YA KAMATI:
Uongozi wa Mfuko umetekeleza agizo hili kupitia barua ya tarehe 22/02/2008 yenye kumbu kumbu namba ZSSF 23/VOL 1/40 iliyopelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyoambana na majibu ya hoja hiyo.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Katika juhudi za kukuza wigo wa Mfuko, Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii unatarajia kujenga nyumba zaidi ya 100 katika eneo la Tunguu, Zanzibar kwa lengo la kuwauzia wanachama wake kwa njia ya mkopo nafuu.

Aidha, Mfuko hauna uwezo wa kuwapatia mikopo wateja wake moja kwa moja isipokuwa katika juhudi za kuwasaidia wateja wake kujikwamua na umasikini, umeazimia kuwadhamini wateja wake wote ili waweze kupata mikopo kupitia Benki mbali mbali zilizopo nchini.

Kamati imepongeza kupokea taarifa hizo na kuutaka Uongozi uharakishe matengezo ya Viwanja vya kufurahishia watoto vilivyopo Unguja na Pemba ili viwe na hadhi inayohitajika na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Mfuko.

8.2 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ):

Agizo:
Benki kulipa kwa wakati madeni yanayodaiwa na Kampuni za watu binafsi. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-161).

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba, mikopo hiyo yenye thamani ya Tsh. 7,156,011,000.00 inajumuisha mikopo ya biashara ya jumla ya Ths.1,626,566,326.00 sawa na asilimia 23 na Tsh. 5,529,444,638.00 sawa na asilimia 77 ni mikopo ya wafanyakazi wa Serikali (personal loans). Aidha, Kamati imefahamishwa kwamba mikopo hiyo tayari imeshalipwa. Hata hivyo, kutokana na utendaji wa shughuli za kibenki, Benki inaendelea kuzidai Taasisi mbali mbali za Serikali na za watu binafsi.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inapendekeza kufutwa kwa hoja hii kwa mnasaba wa maelekezo ya kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za 2005.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Kamati imehoji kuhusu usumbufu wanaoupata wafanyakazi wa Serikali wanaopokelea mishahara yao kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar. Ingawaje katika majibu yaliyotolewa mbele ya Kamati, Uongozi wa Benki umeihakikishia Kamati kwamba usumbufu huo hautakuwepo tena kutokana na Benki kujitahidi kuanzisha 'ATM' na kuongeza vituo 10 kwa mwaka huu hadi kufikia 20 na kuendelea kufungua matawi zaidi ya Benki katika maeneo mbali mbali nchini.

Vile vile Benki imelirejeshea hadhi tawi la Forodhani ili liwe tawi kamili kwa lengo la kupunguza msongamano unaojitokeza. Aidha inakusudia kuanzisha Vituo vya Huduma "Service Centres" katika maeneo ya Wete, Mkoani, Makunduchi na hata sehemu nyengine ya Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kamati imeutaka Uongozi wa Benki kuongeza elimu ya utumiaji wa "ATM" kwa wateja wake, kwani imeonekana kuna tatizo la kukosa uelewa kwa wateja walio wengi.

Benki inatarajia kufungua tawi jengine Dar es Salaam katika jengo linalomilikiwa na Mfanyabiashara Maarufu nchini, Ndg. Said Salim Bakhressa. Jengo hilo limekodiwa kwa miaka kumi na kulipiwa kodi kwa kila mwaka. Hata hivyo, Kamati haikupata Mkataba wake

na wala haijui kiwango cha kodi hiyo. Kamati imeagiza Uongozi wa Benki kupatiwa Mkataba wa jengo hilo.

Kuna tatizo la foleni katika utowaji wa huduma za kila siku za Benki zinazohusiana na
uwekaji na utoaji wa fedha za wateja. Pamoja na sababu nyengine, tatizo hili husababishwa pia na kukosekana kwa wahudumu wakati wa kutolewa huduma hizo. Baada ya suala hili kufikishwa mbele ya Uongozi wa Benki, umelichukua na kulifanyia kazi ili kuondosha kasoro hizo.

Kuhusu Hati Miliki ya Majengo yanayomilkiwa na Benki, Kamati imefahamishwa kwamba, Benki inazo hati hizo kwa majengo yake yote. Kamati imepongeza hali hii na kuutaka Uongozi uendelee kuzitafuta hati hizo kwa majengo yote yatakayomilikiwa na Benki katika siku zijazo.

8.3 BODI YA MAPATO (ZRB):

Agizo Nam.1
Kutafutwa suluhisho juu ya tatizo liliopo la utititri wa ukusanyaji wa kodi Zanzibar. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-343)

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa tatizo hili ni la sera zaidi, hivyo, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeunda Kamati maalum ya “Task Force on Tax Revenue” iliyoundwa na taasisi mbali mbali zikiwemo, Bodi ya Mapato (ZRB); Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); Jumuiya ya Wafanya biashara Zanzibar, Taasisi mbali mbali za Serikali na Asasi mbali mbali za Kiraia, ambayo pamoja na majukumu mengine, pia inashughulikia tatizo hili kila mwaka kabla ya kila kikao cha Bajeti.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, bado Kamati inahisi hili ni tatizo na linahitaji kufanyiwa kazi. Hivyo, Serikali ilichukulie kwa uzito wake ili kuliondosha kabisa.

Agizo Nam. 2:
Kuharakishwa kwa utaratibu wa kuwekwa viwango maalum vya kodi (fixed rates) kwa watalii wa makundi maalum (Package Tours), ili kuepusha udanganyifu unaofanywa na wenye mahoteli kwa kutoa

taarifa za viwango vya chini vya matumizi ya wageni hao. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-343).

MAPITIO YA KAMATI:
ZRB imeanza kuweka 'fixed rates' kwa hoteli hizo na kwa kupitia fedha za wafadhili, imetafuta mshauri mwelekezi ambaye anafanya utafiti "Study" unaohusu Upotevu wa Mapato katika Sekta ya Utalii 'Revenue Loss in Tourism Sector' ili kujua ni kiasi gani cha kodi kinachopotea kutokana na utalii na njia gani zitakazosaidia ili kusaidia ukusanyaji wa mapato. Tayari 'Study' hiyo imeshawasilishwa na kupitiwa na ZRB na baadae itawasilishwa Serikalini kwa mazingatio zaidi.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaendelea kuagiza kukamilika kwa agizo hili ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Agizo Nam.3:
ZRB kuongeza msisitizo wa ulipaji wa kodi wa hiari ili kupunguza tatizo la baadhi ya wafanya biashara kukwepa kodi. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-158).

MAPITIO YA KAMATI:
ZRB inaendelea na utekelezaji wa agizo hili ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kupitia semina, vipindi vya redio, michezo ya kuigiza na makongamano mbali mbali kwa lengo la kuwashajiisha wafanyabiashara juu ya umuhimu wa ulipaji wa kodi kwa khiari.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kuwa agizo hili ni endelevu, ZRB iendelee kulitekeleza kwa ufanisi zaidi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Agizo Nam. 4:
Kuongeza ukusanyaji wa mapato yanayotokana na sekta ya Utalii, msisitizo mkubwa ukiwekwa kwenye hoteli za kiwango cha juu (4-5 Stars). (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-158).

MAPITIO YA KAMATI:
Utekelezaji wa agizo hili unaendelea kutekelezwa ila haujamalizika. Hatua iliyochukuliwa ni kutafuta Mshauri mwelekezi "Enest & Young" ambaye pamoja na mambo mengine atashauri jinsi gani ya kuongeza ukusanyaji wa kodi zitokanazo na Sekta ya Utalii.

MAONI YA KAMATI.
Kamati inahitaji kupewa taarifa za utakelezaji wa agizo hili baada ya kukamilika utafiti wa Mshauri Mwelekezi na kusimamiwa na Bodi.

Agizo Nam. 5:
Kodi ya Uwanja wa Ndege "Airport Safety Fee" kukusanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB). (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-159).

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo hili limetekelezwa kwa ZRB kuanza ukusanyaji wa kodi hiyo tokea mwaka 2009, aidha ukusanyaji wa kodi hii bado unaendelea mwaka hadi mwaka.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza utekelezwaji wa agizo hili.

Agizo Nam. 6:
ZRB kuwasilisha vielelezo vya Hoja Nam. 1.3.1; 1.3.2;1.3.3; na 1.3.4 (2003/04) kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili avikague na baadae kuijuilisha Kamati. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-159)

MAPITIO YA KAMATI:
Vielelezo hivyo vilipelekwa kwa Mdhibiti kupitia barua ya tarehe 21/2/2008 yenye kumbu kumbu namba ZRB/M.30/55 na nakla yake kupelekwa kwa Mwenyekiti na Katibu wa Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inapendekeza kufutwa kwa hoja hii kupitia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005.

Agizo Nam. 7
ZRB kutafuta majibu ya Hoja ya Mdhibiti Nam.13.1.3 inayohusu "Ukwepaji wa Kodi" uliofanywa na mmiliki wa Hoteli ya Vera Club na kutakiwa kulipia adhabu ya USD 105,051.31. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2008/09, uk-37).

MAPITIO YA KAMATI:
Uongozi wa ZRB umeieleza Kamati kwamba, walimuandikia barua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yenye kumbu

kumbu namba ZRB/M.30/Vol.1/63ya tarehe 17 Machi, 2009 ili atoe ufafanuzi jinsi ya deni hilo lilivyofikiwa.
Aidha, Kamati pia ilikutana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupata ufafanuzi wa barua hiyo.

MAONI YA KAMATI:
Maelezo ya ZRB kwamba wanahitaji ufafanuzi wa jinsi ya deni hilo lilivyofikiwa, hayana msingi wowote kwa sababu tayari ufafanuzi umeshatolewa na hatimae kuandikwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti, 2006/07.

Barua ya ZRB kwa Mdhibiti ilikuwa na lugha ya kuagiza, jambo ambalo liko kinyume na Kifungu cha 112 (7) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Pamoja na maelezo haya, Kamati inaiagiza ZRB kutafuta majibu ya hoja hiyo, ili yaweze kupatikana kwa Kamati wakati wowote Kamati itakapoamua kufanya kazi na ZRB.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Masuala ya Kodi zinazotozwa Zanzibar; Ukusanyaji wa kodi na uhusiano wake na Muungano wa Jamhuri ya Tanzania; Ukusanyaji wa Mapato ya ‘Visa’ na Ukusanyaji wa kodi na uhusiano wake na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ni miongoni mwa mambo yanayohitaji uelewa mkubwa na wajumbe wengi wa Kamati hawana ufahamu mpana wa kodi hizo. Hivyo, ni nyema Kamati ikapatiwa elimu zaidi kupitia Semina na njia mbali mbali za kukuza uelewa wao.

Kuna tatizo la magendo ya mafuta linalofanywa na watu mbali mbali kupitia bandari zisizo rasmi zilizopo maeneo tofauti nchini. Hili linapunguza ukusanyaji wa mapato na hivyo, Kamati inaishauri Serikali kulichukulia tatizo hili kwa uzito wake ili kulipunguza na hatimae kuliondosha kabisa, kwani inasemekana Askari wetu pia huhusika katika magendo hayo.

8.4 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR:

Agizo Nam.1:
Shirika kuongeza hisa katika soko la Bima la Tanzania hususan katika sekta ya viwanda, Mizigo, Meli na Mahoteli ambayo hivi sasa

yanaonekana kuongezeka nchini. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-152).

MAPITIO YA KAMATI:
Shirika linaendelea kutekeleza agizo hili kwa kutanua wigo wake wa biashara kwa kufungua Afisi zake za kanda Mbeya na Dodoma. Aidha, pamoja na kuongezeka kwa ushindani wa biashara kutokana na kuongezeka kwa Makampuni ya Bima Tanzania, wastani wa soko umeongezeka na kufikia asilimia nne (4%) kiwango kilicho juu zaidi ya "industrial average market share" ambayo ni asilimia 3.7%.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imefurahishwa na hatua hii na kulitaka Shirika liendeleze juhudi hizo ili kukuza soko.

Agizo Nam.2:
Shirika kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili kuongeza idadi ya wateja wa Shirika. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-152).

MAPITIO YA KAMATI:
Juhudi zinaendelea ikiwa ni pamoja na uchapishaji wa vipeperushi na 'folders'. Kutoa elimu kupitia vyombo vya habari pamoja na kutoa kalenda za ukutani, kuwatembelea wateja wakubwa wa Shirika na kuzungumza nao juu ya mambo mbali mbali yanayohusiana na Bima. Jitihada hizi zimelisaidia Shirika kukuza mapato yake kutoka 5,573,694,300 kwa mwaka 2007 hadi kufikia Tsh. 8,368,526,400 kwa mwaka 2009.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza juhudi zilizochukuliwa, ila inashauri juhudi zaidi zichukuliwe ili kuongeza idadi ya wateja wa Shirika.

Agizo Nam.3:
Shirika kuchukua juhudi za makusudi kupunguza gharama ili kumudu ushindani na kuongeza faida. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-153).

MAPITIO YA KAMATI:
Shirikia limefanya juhudi hizo ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya wafanyakazi 26, kuwatumia Mameneja wa kanda walio karibu ili

kupunguza safari za kikazi Mikoani; kupunguza kulipa muda wa ziada wa saa za kazi pasi na ulazima (over time) na kupunguza matumizi yasiyo la lazima. Kwa kufanya hivyo, Shirika limeweza kutengeneza faida kutoka Tsh.1,767,808,954 kwa mwaka 2007 hadi Tsh.106,948,876 kwa mwaka 2009.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza mafanikio hayo na kulitaka Shirika kuendeleza juhudi za kuongeza faida.

Agizo Nam.4
Shirika kulishughulikia tatizo la kutolipwa kwa "Primium" kwa wakati na kufuatilia deni la Madalali na Mawakala wote waliohusika kwa kuwafutia leseni za biashara ya Bima na kuzifunga Ofisi zao. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2007/08, uk-153).

MAPITIO YA KAMATI:
Matatizo hayo sasa yamepatiwa dawa kwa kuwepo Sheria mpya ya Bima ya mwaka 2009. Aidha, Shirika pia limechukua juhudi za kuwapanga wakaguzi wa kupita kwa Mawakala kwa kuwakagua mara kwa mara ili kuona utendaji wao. Shirika pia limechukua hatua za kuzifunga ofisi sita na kutafuta Mawakili kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kulipwa kwa Tsh. 56,000,000/- na hivyo kupunguza madeni hayo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inapongeza juhudi zilizochukuliwa na kulitaka Shirika liendelee kufuatilia zaidi.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:
Kamati ilihoji taratibu za kisheria zilizotumika katika zoezi la kuwapunguza uliofanywa wa Shirika na kufahamishwa kwamba, Shirika lilifanya utafiti "Study" kabla ya upunguzaji huo na hatimae kuwapunguza wahudumu na walinzi, kama taratibu za sehria zinavyoelekeza na badala yake kuajiri Makampuni binafsi kwa bei nafuu zaidi kulinganisha na mishahara waliyokuwa wakilipwa wafanyakazi hao.

Kuhusu Tawi la Dodoma, Shirika limo mbioni kufungua tawi hilo kwa matarajio ya kupata faida na kuongeza wigo wa biashara. Kwa mnasaba na hili, Kamati imefahamishwa kwamba, 80% ya mapato ya Bima yanatoka Tanzania bara, kati ya hizi, 60% yanakusanywa Mkoa wa Dar es Salaam peke yake, na 20% hukusanywa kwa

Matawi ya Mbeya, Arusha na Mwanza. Bila ya shaka kuanzishwa kwa tawi la Dodoma kutasaidia zaidi katika ukusanyaji huo.

9.0 WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI:

Agizo Na. 1:
Upatikanaji wa ramani halisi za mashamba yaliyovamiwa (Kijichi, Kituo cha Urafiki, Kizimbani na Selemu) pamoja na hati miliki za mashamba hayo. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-92).

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo hili bado halijamaliza utekelezaji wake. Wizara imeshawasilisha maombi ya kupatiwa hati miliki katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ikiwa ni pamoja na kufanya 'survey' ya eneo hilo kwa lengo la kupatikana ramani halisi inayohitajika.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, Kamati imetaka kujiridhisha kwa kupatiwa kwa maandishi juhudi zilizochukuliwa katika kudai hati miliki ikiwa ni pamoja na barua ya mawasiliano baina ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Mpaka tunaandika ripoti hii, ushahidi huo bado haujawasilishwa kwa Kamati.

Kamati pia imekusudia kukutana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ili kupata ufafanuzi wa Upatikanaji wa Hati Miliki kwa Taasisi za Serikali.

Agizo Nam.2:
Wizara kuchukua hatua za umiliki wa Shamba la Makurunge liliopo Bagamoyo na kuwa mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Chuo cha Kilimo, Kizimbani. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2009/2010, uk-109).

MAPITIO YA KAMATI:

Wizara inaendelea na kulifuatilia suala hili. Baada ya kuchukua hatua ya kumwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kuhusu umilikishwaji wa shamba hilo chini ya Chuo cha Kilimo, Kizimbani kama makubaliano haya yalivyoahidiwa mbele ya Kamati ya mwaka 2009/2010, Wizara

ilipokea barua ya majibu ya kukatisha tamaa na hatimae Wizara kwa mara nyengine ikalazimika kumuandikia tena barua ya kumtaka aheshimu maamuzi ya Serikali Kuu ya kuwapatia Chuo cha Kilimo hati miliki ya shamba hilo. Hivyo, Wizara sasa inasubiri majibu ya barua hiyo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza hatua hiyo na kuisisitiza Wizara kuendelea kudai Hati Miliki huku Wizara ikiijuilisha Kamati hatua itakazofikia.

Agizo Nam. 3:
Upatikanaji wa Matrekta kama yalivyokadiriwa kwenye Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2006/2007. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-327).

MAPITIO YA KAMATI:
Jumla ya matrekta 12 yalinunuliwa kwa mwaka wa 2009/2010. Matrekta 2 yalikabidhiwa Taasisi za Serikali ikiwemo JKU na Idara ya Anga, 6 yalibaki Unguja na 4 yalipelekwa Pemba kwa matumizi ya kazi za kilimo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza juhudi hizo ila inasisitiza Wizara iyatunze matrekta hayo na huku ikiendelea kutafuta matrekta mengine.

Agizo Nam.4:
Wizara kuimarisha miradi na vitengo vyake vya utafiti ili kutokomeza maradhi ya matunda. (Agizo hili linatokana na Ripoti ya Kamati, 2006/07, uk-327).

MAPITIO YA KAMATI:
Agizo hili linaendelea kutekelezwa. Wizara imejitahidi kuweka mitego mbali mbali kuzuia uharibifu wa wadudu hususan wa embe na kufanikiwa kupunguza kutoka asilimia 75% hadi 43%. Aidha, Wizara inawahamasisha wakulima kukusanya matunda yenye mafunza na kuyazika, kutumia dawa mpya ya kunyunyiza (success bait) na kuongeza mitego ya ziada hadi kufikia 40,000/- ili itosheleze kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza kuendelea kwa jitihada hizo na kuitaka Wizara iendelee kupambana na tatizo hili, ili liweze kuondoka moja kwa moja.

MAMBO MENGINE YALIYOJITOKEZA:

Kamati pamoja na kupata ufafanuzi huo, imeazimia kutembelea Chuo cha Kilimo, Kizimbani ili kufahamu kwa kina namna Wizara inavyokiendeleza Chuo hicho na hatimae kuweza kutumika kuondosha matatizo mengi yanayowakabili wakulima.

Kamati imehitaji na hatimae kukabidhiwa Mikataba ya Maghala "Go-downs" yanayomilikiwa na Wizara na kukodishwa kwa Makampuni binafsi. Kamati inahitaji kupata muda wa kutosha wa kukaa na Wizara ili kuipitia mikataba hiyo na hatimae kutembelea maghala hayo. Hata hivyo, Kamati imehitaji kupatiwa orodha ya vyanzo vya mapato vya Wizara ili ipate ufafanuzi wake. Mpaka tunaandika ripoti hii, suala hili Kamati bado haijapatiwa vyanzo hivyo.

SEHEMU YA TATU:

10.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO:

Kamati inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Wizara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kwa mashikiano makubwa waliyoyaonesha wakati wote wa kazi za Kamati. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirkiano mazuri waliyoipa Kamati wakati wote, aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Afisi hii kwa kuiandalia mafunzo Kamati kuhusu mada mbali mbali kwa lengo la kuiwezesha Kamati kutekeleza vyema majuku yake.

Kamati ya kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mshirika inatekeleza majukumu mazito ya udhibiti na uchunguzi wa matumizi sahihi ya fedha za umma kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu, kazi hizi hazingeweza kutelezwa kwa ufanisi kutokana na muda mdogo unaotolewa kwa Kamati. Kamati inaendelea kuitaka Serikali iliwezeshe zaidi Baraza la Wawakilishi, ili Kamati zake nazo zipate uwezo wa kutekeleza vyema majukumu yao.

Kamati inakumbushia tena tatizo inalokabiliana nalo la kuhitaji uelewa mpana wa masuala ya fedha na hivyo ipatiwe mafunzo yanakayoiwezesha kutekeleza vyema majukumu yake. Masuala ya fedha ni mazito na yanahitaji uelewa mkubwa sana na takriban Wajumbe wa Kamati hawana wigo mpana wa kufahamu mbinu za kifedha. Kwa kuwa Kamati ndiyo yenye kazi ya kuchunguza na kuzidhibiti mali za Serikali, tunaishauri Serikali ilitizame kwa jicho

la karibu suala hili ili kukuza utendaji kazi wa Kamati. Tunapenda kuzipongeza Afisi ya Baraza la Wawakilishi, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuazimia kuipatia mafunzo Kamati na tunazitaka zikamilishe utekelezaji wa ahadi hizi.

Kamati inaendelea kuitakaSerikali iifuatilie Ripoti ya Kamati na kuyatekeleza kwa vitendo maagizo ya Kamati ili kupunguza malalamiko ya Wajumbe wa Baraza kwamba, Ripoti za Kamati zinadharauliwa. Kwa mfano kifungu cha 51 (7) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, kinamtaka Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha, uchumi na Mipango ya Maendeleo kuwajibika katika kuifuatilia na kutekeleza mapendekezo yote ya Kamati na kuijuilisha Kamati juu ya utekelezaji wake wa hatua hizo. Kinachoisikitisha Kamati ni kwamba, hakuna utekelezaji huo na matokeo yake Kamati imekuwa ikitoa ripoti ya mambo hayo hayo kila mwaka huku Serikali haionekani kuwa tayari kuyafanyia kazi.

Jambo jengine ambalo Kamati inapenda kulikumbusha ni kufanya mabadiliko ya Sheria za Fedha na zaidi katika kipengele cha adhabu. Sheria zetu za fedha zimeonesha adhabu ila adhabu hiyo haiendani na wakati husika ama ni ndogo kulinganisha na makosa yanayofanyika. Kwa mfano, kifungu cha 38 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sheria Namba. 12 ya mwaka 2005, kimetoa adhabu mbili kuu ambazo inaweza kutekelezwa moja ama zote. Adhabu ya kwanza iliyotolewa kwa anaekiuka sheria hiyo ni kupigwa faini kwa kutozwa fedha zisizozidi Laki tano baada ya kutiwa hatiani. Hii ni adhabu ndogo sana kwa mtendaji ama mtu aliyejikusanyia Mabilioni ya fedha za umma kwa manufaa binafsi. Aidha kifungu hicho kimeendelea kutaja adhabu ya kifungo kwa mkiukaji wa Sheria hiyo kwa anaeshtakiwa na kutiwa hatiani ni kutumikia kifungo kisichozidi miaka 2. Ama hata ikiamuliwa kutumikia adhabu zote mbili, basi haiwi sababu ya kumuogopesha mtu kufanya makosa, matokeo yake atafanya makosa huku akiamini hatua kubwa itakayochukuliwa ni kuhamishwa Ofisi moja na kupelekwa nyengine na kule pia anafanya mambo yale yale, kama vile ilivyotokea kwa aliyekuwa Mhasibu wa Shirika la Huduma za Maktaba ambae tumeshatoa maelezo yake katika ripoti hii. Tunaomba Sheria za fedha zipitiwe tena na ikiwezekana zitoe adhabu ya kila kifungu kinachohusika na isiwe kwa ujumla kama ilivyo, na adhabu hiyo ilingane na wakati na uhalisia wa kosa lenyewe.